Kupata Furaha Katika Ubatili Wa Maisha

(Finding Joy in the Vanity of Life)

na

Ellis P. Forsman

Kupata Furaha Katika Ubatili Wa Maisha

na

Ellis P. Forsman

Octoba 11, 2011

Kupata Furaha Katika Ubatili Wa Maisha

Mhu. 2:22-24

Kitabu kinachovutiakatika Biblia ni Mhubiri.

Zimetolewa sifa nyingi kwa Sulemani.

- Mhu. 1:1, "*Maneno ya Mhubiri mwana wa Daudi mflame katika Yerusalemu.*"
- Mhu. 1:12, "*Mimi mhubiri nalikuwa mfalme wa Israeli katika Yerusalemu.*"

Mwandishi anaelezea utafutaji wake kwa kumanisha katika maisha. Mhu. 1:13, "*Nikatia moyo wangu ili kuyatafuta yote yanayotendeka chini ya mbingu, na kuyavumbua kwa hekima; ni taabu kubwa ambayo Mungu amewapa wanadamu, ili kutaabika ndani yake.*"

Utafutaji wake katika maisha "chini ya jua". Neno lililotumikwa mara 29 katika mistari 27; hupendekezaa kutazama maisha kutoka katika mzamo wa kindani wa dunia. Mhu. 1:3, "*Mtu ana faida gani ya kazi yake yote aifanyayo chini ya jua?*"

Ujumbe wake unaweza kuonekana tofauti.

Maandhari ni ubatili wa maisha (ubatili umetumiwa mara 35 katika mistari 29).

- Mhu. 1:2, "*Mhubiri asema, ubatili mtupu, ubatili mtupu, mambo yote ni ubatili.*"
- Mhu. 1:14, "*Nimeziona kazi zote zifanywazo chini ya jua; na tazama mambo yote ni ubatili naa kujilisha upepo.*"

Alafu anataja maneno kama furaha (3), kufurahia (3), starehe (2), furahia (4), na furaha (1). Hakika, kitabu hiki kinatoa ushauri jinsi ya kuenenda katika maisha yetu…kupata furaha katika maisha ambayo ni ubatili! Mhu. 2:22-24, "*Kwa maana mtu hupata nini kwa kazi yake yote, na kwa juhudi ya moyo wake alivyojitahidi chini ya jua? Kwa kuwa siku zake zote ni masikitiko, na kazi yake ni huzuni; naam, hata usiku moyoni mwake hamna raha. Hayo nayo ni ubatili. Mwana damu hapati jema kupita kula na kunywa, na*

kuiburudisha roho yake kwa mema katika kazi yake. Hayo nayo naliona ya kwamba hutoka mkononi mwa Mungu."

Kupata furaha kama hiyo, mtu ni lazima akumbane na ukweli wa…

Ubatili wa maisha

Ujuzi wa mhubiri.

Ubatili wa starehe. Mhu. 2:1, "*Nikauambia moyo wangu haya, nitakujaribu kwa njia ya furaha basi ujifurahishe kwa anasa. Na tazama hayo nayo yakawa ubatili.*"

Ubatili wa kiwanda (kazi).

- Mhu. 2:11, "*Kisha nikaziangalia kazi zote zilizofanywa kwa mikono yangu, na taabu yote niliyotaabika katika kuzitenda; na tazama yote ni ubatili na kujilisha upepo wala faida hakuna chini ya jua.*"
- Mhu. 2:22-23, "*Kwa maana mtu hupata nini kwa kazi yake yote na kwa juhudi wa moyo wake alivyojitahidi chini ya jua? Kwa kuwa siku zake zote ni masikitiko, na kazi yake ni huzuni; naam, hata usiku moyoni mwake hamna raha. Hayo nayo ni ubatili.*"
- Mhu. 4:4, "*Tena nikafikiri amali zotena kila kazi ya ustadi, yaa kwamba inatoka katika mtu kupingana na mwenzake. Hayo nayo ni ubatili na kujilisha upepo.*"

Ubatili wa hekima ya mwanadamu. Mhu. 2:15, "*Nikasema moyo wangu, kama limpatavyo mpumbavu, ndivyo litakavyonipata mimi nami; basi kwa nini nikawa na hekima zaidi? Nikasema moyoni mwangu ya kuwa hayo nayo ni ubatili.*"

Ubatili wa maisha yote. Mhu. 2:17, "*Basi nikauchukia uhai; kwa sababu kazi inayotendeka chini ya jua ilikuwa mbaya kwangu; yaani mambo yote ni ubatili na kujilisha upepo.*"

Ubatili wa kuacha urithi. Mhu. 2:18-21, "*Nami nikaichukia kazi yangu yote niliyojishughulisha nayo chini ya jua; maana sina budi kumwachia yeye atakayenifuata. Naye ni nani ajuaye kama huyo atakuwa mwenye hekima au mpumbavu? Hata hivyo atatawala juu ya kazi yangu yote niliyojishughulisha nayo, ambamo ndani yake mimi nimeonyesha hekima chini ya jua. Hayo nayo ni*

ubatili. Kwa hiyo nikageuka kukata tamaa moyoni mwangu juu ya kazi yangu yote niliyojishughulisha nayo chini ya jua. Maana kuna mtu ambaye kazi yake ni kwa hekima, na kwa maarifa, na kwa ustadi; naye atamwachia mtu asiye shughulika nayo kuwa sehemu yake. Hayo tena ni ubatili, nayo ni baa kuu."

Uchunguzi wa mhubiri

Ubatili wa kuwepo duniani. Mhu. 3:19-21, "*Kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama; jambo moja lawatukia; anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu; naam, wote wanayo pumzi moja; wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyaama; kwa maana yote ni ubatili. Wote huendaa mahali pamoja; wote hutoka katika mavumbi; na hata mavumbini hurudi tena. Ni nani ajuaye kama roho ya binadamu huenda juu, na kama roho ya mnyama huenda chini?*"

Ubatili wa kutaka utajiri kuliko familia. Mhu. 4:7-8, "*Kisha nikarudi tena na kuona ubatili chini ya jua. Kuna mtu aliye pekee yake wala hana wa pili wake; naam, hana mwana wala ndugu; hata hivyo amali yake haina mwisho, wala macho yake hayashibi utajiri. Basi asema ni kwa ajili ya nani nafanya kazi, na kujinyima nafsi yangu mema? Hayo nayo ni ubatili, naam, ni tabu kubwa.*"

Ubatili wa umaarufu wa kisiasa. Mhu. 4:16, "*Hawakuwa na kikomo hao watu wote, hao wote ambao alikuwa juu yao; lakini hata hivyo wale wafuatao baada yake hawatamfurahia. Hakika hayo pia ni ubatili, na kujilisha upepo.*"

Ubatili wa ndoto nyingi na maneno mengi. Mhu. 5:7, "*Maana ndivyo ilivyo katika habari za wingi wa ndoto, na ubatili, na maneno mengi; walakini wewe umche Mungu.*"

Ubatili wa kupenda vingi. Mhu. 5:10, "*Apendaye fedha hatashiba fedha, wala apendaye wingi hatashiba nyongeza.*"

Ubatili wa utajiri pasipo karama ya Mungu kuifurahia. Mhu. 6:2, "*Mtu aliyepewa na Mungu mali, ukwasi, na heshima, hata asipungukiwe na kitu cho chote kwa nafsi yake katika yote anayoyatamani walakini Mungu hamwezeshi kula katika hizo; bali mgeni hula. Nayo ndiyo ubatili hasa, nayo ni ugonjwa mbaya.*"

Ubatili wa tamaa ya kutangatanga. Mhu. 6:9, "*Heri kuona kwa macho, kuliko kutangatanga kwa tamaa. Hayo nayo ni ubatili, na kujilisha upepo.*"

Ubatili wa kicheko cha kipumbavu. Mhu. 7:6, "*Maana kama mlio wa miiba chini ya sufuria, ndivyo kilivyo kicheko cha mpumbavu. Hayo nayo ni ubatili.*"

Ubatili wa kutokuwa na haki katika maisha haya. Mhu. 8:14, "*Kuna ubatili unaofanyika juu ya nchi, kwamba wako wenye haki nao hupatilizwa kama kwa kazi yao maovu; tena wako waovu nao wapatilizwa kama kwa kazi yao wenye haki. Nami nikasema ya kuwa hayo nayo ni ubatili.*"

Ubatili wa siku zenye giza. Mhu. 11:8, "*Naam, mtu akiishi miaka mingi na aifurahie yote; lakini na azikumbuke siku zijazo za giza kwa maana zitakuwa nyingi. Mambo yote yajayo ni ubatili.*"

Ubatili wa utoto na ujana. Mhu. 11:10, "*Kwa hiyo ondoa majonzi moyoni mwako, nawe uuondoe ubaya mwilini mwako; kwa maana ujana ni ubatili, na utu uzima pia.*"

Hitimisho la mhubiri

Kama ilivyoelezwa kwenye utangulizi. Mhu. 1:2, "*Mhubiri asema, ubatili mtupu, ubatili mtupu, mambo yote ni ubatili.*"

Akielekea kuelezea ufuatiliji wake wa kumanisha. Mhu. 1:14, "*Nimeziona kazi zote zifanywazo chini ya jua; na tazama mambo yote ni ubatili na kujilisha upepo.*"

Watu wengi wamefikia hitimisho kama hili na wakaangukia katika uharibifu na kukata tamaa. Pia Mhubiri angetutaka tujifunze na kufahamu jinsi ya kupata furaha ya kweli katika maish.

Furaha katika maisha

Uzoefu wa mhubiri.

Moyo wake ulifura katika kufanya kazi. Mhu. 2:10, "*Wala sikuyanyima macho yangu chochote yalichokitaamani; wala sikuuzuia moyo wangu katika furaha yo yote; maana moyo wangu ulifurahi kwa sababu ya kazi yangu yote, nah ii ilikuwa sehemu yangu katika kazi yangu yote.*"

Zaawadi ya kazi yake ilikuwa ni furaha ya kuifanya. Mhu. 2:10, "*Wala sikuyanyima macho yangu chochote yalichokitaamani; wala sikuuzuia moyo wangu katika furaha yo yote; maana moyo wangu ulifurahi kwa sababu ya kazi yangu yote, nah ii ilikuwa sehemu yangu katika kazi yangu yote.*"

Uchunguzi wa mhubiri.

Hakuna kitu bora kama kuyafurahia vitu rahisi na kile ufanyalo. Mhu. 2:24, "*Mwanadamu hapati chema kupita kula na kunywa, na kuiburudisha roho yake kwa mema katika kazi yake. Hayo nayo naliona ya kwamba hutoka mkononi mwa Mungu.*"

Uwezo wa kukifurahia ulichonacho na kile ufanyalo hutoka kwa Mungu. Mhu. 2:24-25, "*Mwanadamu hapati chema kupita kula na kunywa, na kuiburudisha roho yake kwa mema katika kazi yake. Hayo nayo naliona ya kwamba hutoka mkononi mwa Mungu. Kwa maana ni nani awezaye kula au kujiburudisha kuliko mimi?*"

Mungu anatoa hekima, maarifa, na furaha kwa mwanadamu mwema machoni pake. Mhu. 2:26, "*Kwa sababu Mungu humpa yeye aliyemridhia hekima na maarifa na furaha; bali mkosaji humpa taabu, ili kukusanya na kututa, apate kumpa huyo ambaye Mungu amridhia. Hayo nayo ni ubatili na kujilisha upepo.*"

Muovu anaweza kuhitaji vingi, lakini mara watapewa wema. Mhu. 2:26, "*Kwa sababu Mungu humpa yeye aliyemridhia hekima na maarifa na furaha; bali mkosaji humpa taabu, ili kukusanya na kututa, apate kumpa huyo ambaye Mungu amridhia. Hayo nayo ni ubatili na kujilisha upepo.*"

Mwanadamu anapaswa kufurahi na kutenda mema. Mhu.3:12, "*Mimi najua ya kuwa hakuna jema kwako kupita kufurahi, na kufanya mema maadamu wanaishi.*"

Kila mwanadamu anapaswa kufurahia mema katika kazi zao, ambayo ndio zawadi toka kwa Mungu. Mhu.3:13, "*Tena ni karama ya Mungu kila mtu apate kula na kunywa, na kujiburudisha kwa mema katika kazi yake yote.*"

Furaha katika kazi ya mtu ndio urithi wake, siyo kitakachotokea akishaondoka. Mhu.3:22, "*Hivyo nikaona ya kwamba hakuna jema kupita mwanadamu kuzifurahia kazi zake; kwa sababu hili ni fungu lake; kwa maana ni nani atakayemrudisha tena ili ayaone yatakayomfuata badaye.*"

Tena, hii ni urithi wa mtu, na ni zawadi toka kwa Mungu. Mhu.5:18-20, "*Tazama mimi niliyoyaona kuwa ndiyo mema na ya kufaa ni mtu kula na kunywa, na kujiburudisha katika mema kwa kazi yake yote anayoifanya chini ya jua, siku zote za maisha yake alizopewa na Mungu; maana hilo ndilo fungu lake. Tena kwa habari za kila mwanadamu ambaye Mungu amempa mali na ukwasi,*

akamwezesha kula katika hizo, na kuipokea sehemu yake na kuifurahia amali yake; hiyo ndiyo karama ya Mungu. Kwa kuwa mtu hatazikumbuka mno siku za maisha yake; kwa sababu Mungu humtakabali katika furaha ya moyo wake."

Hivyo katika siku ya mafanikio, fuarahi; na siku mbaya, tafakari. Mhu.7:14, "*Siku ya kufanikiwa ufurahi, na siku ya mabaya ufikiri. Mungu ameifanya hiyo moja kwenda sambamba na hiyo ya pili, ili mwanadamu asipate kulijua neno lolote litakalofuata baada yake.*"

Hivyo anashauri furaha ya matunda ya kazi ya mtu. Mhu. 8:15, "*Kisha nikaisifu furaha, kwa sababu mwanadamu hana neno lolote lililojema chini ya jua, kuliko kula, na kunywa, na kucheka; nay a kuwa hilo likae naye katika amali yake, siku zote za maisha yake alizompa Mungu chini ya jua.*"

Hitimisho la mhubiri.

Kula na kunywa kwa moyo wenye furaha. Mhu.9:7, "*Wewe enendaa zako ule chakula chako kwa furaha, unywe mvinyo yako kwa moyo wa kuchangamka kwa kuwa Mungu amekwisha kuzikubali kazi zao.*"

Onyesha furaha yako kwa jinsi unavyoishi. 9:8, "*Mavazi yako nay awe meupe sikuzote; wala kichwa chako kisikose marhamu.*"

Ishi kwa furaha na mke wako ambaye unampenda. Mhu. 9:9, "*Uishi kwa furaha pamoja na mke umpendaye, siku zote za maisha yako ya ubatili, ulizopewa chini ya jua; siku zote za ubatili wako, kwa maana huo ni sehemu yako ya maisha; na katika taabu zako ulizozitaabika chini ya jua.*"

Furahia ujana wako, alafu kumbuka utakuwa na hatia. Mhu.11:9, "*Wewe kijana uufurahie ujana wako na moyo wako ukuchangamshe siku za ujana wako, ukaziendee njia za moyo wako, na katika maono ya macho yako, lakini ujue wewe ya kwamba kwa ajili ya hayo yote Mungu atakuleta hukumuni.*"

Hivyo basi, ondoa huzuni na kuweka mbali uovu, maana ujana una maisha mafupi. Mhu.11:10, "*Kwa hiyo ondoa majonzi moyoni mwako, nawe uondoe ubaya mwilini mwako, kwa maana ujana ni ubatili, na utu uzima pia.*"

Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako. Mhu.12:1, "*Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka utakaposema, mimi sina furaha katika hiyo.*"

Muogope Mungu na shika maagizo yake, maana hili ndio kusudi lako la kuinshi. Mhu.12:13, "*Hii ndiyo jumla ya maneno yote yamekwisha sikiwa; mche Mungu nawe uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu.*"

Hitimisho

Maisha "*chini ya jua*" ni ubatili. Bila Mungu, hakuna maana ya maisha. Bila Mungu, hautafurahia muda wako duniani.

Maisha "*chini ya jua*" inaweza kujawa na ujuzi wenye furaha pamoja na kumbukumbu yenye furaha. Pamoja na Mungu kutuongoza katika kuweka vipaumbele vyetu vikiwa vimenyooka. Mungu kutubariki kwa hekima na uwezo wa kufurahi kunafuraha iliyoje katika maisha.

Kupata furaha katika ubatili wa maisha, mkumbuke Muumba wako, mtii Mungu, tunza sheria zake. Hasa leo, hiyo inamanisha kumsikiliza mwanaye na mwokozi. Heb. 1:1-4, "Mungu ambaye zamani alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka awe mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufaanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; amefanyika bora kupta malaika kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao."